

Machi 2017



Wapendwa marafiki,

Mwezi huu tunasherekea na wanawake wote kama sehemu ya Siku ya Wanawake duniani. Ujumbe wa sikukuu hiyo kwa mwaka huu unasema “Uwe jasiri kwa ajili ya mabadiliko.”

Nilianza kufikiria wanawake wa kiBiblia waliokuwa jasiri kwa ajili ya mabadiliko. Waliishi kwa ajili ya Mungu na kuwatumikia watu kwa vipaji na matendo. Mwanamke mmoja anayenijia akilini ni Debora nabii- mwamuzi tunayempata kwenye kitabu cha Waamuzi (4:1–24).

Debora ndio mwanamke pekee mwaamuzi anayetajwa kwenye Biblia. Alimwambia Baraka kuwa Mungu amemuamuru kuongoza mashambulizi dhidi ya vikosi vya mfalme. Baraka alisita kumtii Mungu, lakini Debora alimkumbusha ahadi ya Mungu kwa ujasiri. Debora alikuwa mwanamke jasiri kwa ajili ya mabadiliko.

Inatugharimu nini ili kuwa wanawake jasiri kwa ajili ya mabadiliko? Tuko tayari kuwa sauti ya wanawake wasiokuwa na sauti? Kupigania mabadiliko ya wanawake wanaonyanyaswa na kutelekezwa kwenye baadhi ya maeneo ulimwenguni sasa hivi? Kuomba na kutafuta hekima na nguvu za Mungu na kusimama kwa ajili ya wanaonyamazishwa na kuteswa?

Kila mwanamke ameumbwa kwa mfano wa Mungu. Tusimame pamoja tunapomba kwa ujasiri kwa ajili ya mabadiliko. Tuwe wanawake wanaoweza kusema tunamuamini Mungu na tunajua kuwa yeye ni Mungu wa miujiza. Tuwe wanawake wanaoamini kuwa Mungu anaona kinachotokea kwa dada zetu wanaokandamizwa. Wanawake wanaoutoa muda, talanta na rasilmali zao kusaidia kuzibadilisha jamii, miji, na nchi kwa ajili ya Kristo.

Leo, mnapokutana kwa ajili ya kuomba, ungana na maombi ya wanawake ulimwenguni kote wanaoomba pamoja kwa ajili ya mabadiliko. Unahitaji wapi ujasiri zaidi? Mungu anakuita kuzungumza na nani ili kumkumbusha ahadi za Mungu kwa ajili ya maisha yao leo?

Nyinyi ni binti zake, walioitwa kuomba na kuwa jasiri kwa ajili ya mabadiliko kwenye mioyo ya wanawake ulimwenguni kote. Moyo wangu unaumia pamoja na wa kwako tunapokuwa jasiri kwa ajili ya injili tukitumaini kuwa mioyo mingi imeunganishwa pamoja na moyo wa Mungu kupitia kwa mwanaye Yesu.

Katika yeye, mioyo yetu inashangilia,

Peggy Banks

Mkurugenzi wa Huduma Ulimwenguni

TWR Wanawake wa Matumaini/Project Hannah